# VITABU VITANO VYA MUSA

Na Dan R. Owen

Vitabu vitano vya Biblia, vinajulikana kama Sheria, viliandikwa na Musa nabii mkubwa wa Mungu (Yohana 1:17). Vitabu hivi vimeanza na uumbaji wa ulimwengu na vinamalizia na kifo cha Musa.Vimejaa masimulizi ya wema wa Mungu na uovu wa wanadamu,uvumilivu wa Mungu na Ukaidi wa mwanadamu. na uhaba wa imani kwa wanadamu.

Wakati Mungu alipoumba ulimwengu, Mungu aliona kila kitu alichokifanya “na tazama, ni chema sana,” (Mwanzo 1:31).Mungu alimumba mwanaume na mwanamke kwa mfano wake na kuwaweka katika bustani ya furaha (Mwanzo 1:26:2:8-15).Kila kitu kilikuwa chema mpaka walipo muasi Mungu na kuondolewa katika bustani (Mwanzo 3). Maumivu,magonjwa na kifo vilikuja ulimwenguni kwa sababu ya dhambi (Mwanzo 3:16-17).Na baada ya wanadamu wa kwanza kuondolewa katika bustani ya Edeni, Uovu ulianza kuenea katika ulimwengu. Machafuko na kutokutii Mungu kuliongezeka mpaka Dunia ikajawa na uovu.

Na hata katika ulimwengu mkaidi, baadhi ya watu huchagua kumtii Muumba wao,Habili alimuabudu Mungu kama Mungu alivyomuagiza (Mwanzo 4:2-4). Henoko alitembea sawa sawa na amri za Mungu, na Nuhu alikuwa mtu mwenye haki aliyetembea na Mungu (5:20; 6:9). Mungu aliwabariki wale waliojaribu kufanya mapenzi yake. Wakati alipouangamiza ulimwengu wote kwa gharika kuu, alimuokoa Nuhu na familia yake (Mwanzo 6-8). Nuhu bado ni mfano mkubwa kwa wale wachache waliochagua kumtii Mungu (Waebrania 11:7)!

Baada ya kipindi cha Nuhu, Mungu aliutawanya uzao wa Nuhu Duniani kote. Moja ya uzao wa Nuhu ulikuwa ni mtu aliyeitwa Abrahamu. Kama Henoko na Nuhu kabla yake,Abrahamu alitembea na Mungu, akimuamini Mungu na kufanya kila alichoamriwa na Mungu kukifanya. Mungu alifanya ahadi kubwa na Abrahamu. Aliahidi kumbariki Abrahamu, na kumfanya kuwa taifa kubwa kupitia uzao wake,na siku moja, kuwabariki mataifa yote ya ulimwengu kupitia vizazi vyake (Mwanzo 12:1-3).Masimulizi yanayoendelea ka tika kitabu cha Mwanzo ni jinsi ambavyo Mungu alimbariki Abrahamu watoto na wajukuu zake, na jinsi ambavyo Mungu alianza kulikuza taifa kubwa la Israeli.Abrahamu alipata mtoto akiwa mzee akamuita jina lake Isaka. Isaka akawa na mtoto akamuita jina lake Yakobo. Yakobo akawa na wana kumi na mbili ambaye alikuwa ni baba wa kabila 12 za Israeli. Kipindi cha njaa kubwa, wakati familia ya Yakobo ilipokosa tumaini na kukataliwa, Mungu aliwafanya watu wake wapelekwe Misri ambako kuna chakula. Watu sabini wa familia ya Yakobo waliondoka nchi ya Kanaani na kuelekea Misri (Mwanzo 46:27).

Kitabu cha Kutoka hutueleza jinsi familia ya Yakobo (ambayo pia iliitwa aiWaraeli) ilivyofanyika kuwa taifa kubwa.Kipindi cha miaka 400 ya utumwa wakiwa Misri, watu wa Israeli waliongezeka. Walipata wanaume 603,550 wenye uwezo wa kupigana, wanawake na watoto. Mungu akamtuma nabii, Musa, akitaka watu wake waachiwe toka utumwani. Farao wa Misri alikataa kuwachia waende! Akasema, "BWANA ni nani, hata niisikilize sauti yake,na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui BWANA,wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao"! (Mwanzo 5:2). Mungu alituma mapigo kumi juu ya taifa la Misri na kumfanya Farao abadili mawazo yake na kumuonyesha uweza wake. Hatimaye, ndipo wakati Mungu alipouwa kila mzaliwa wa kwanza katika Misri,Farao akawaachia huru wana wa Israeli (Mwanzo 12:14).

Kitabu cha kutoka kinatueleza jinsi wana wa Israeli walivyo ondoka Misri na kusafiri hadi mlima Sinai. Hapo, Mungu alijifunua mwenyewe kwa Musa na kuwapa wa Israeli sheria zake. Mungu alitoa nafasi ya kuwa na uhusiano wake kama watamtii (Mwanzo 19:5-6). Watu walikubali kufanya mapenzi ya Mungu na Agano kati ya Mungu na wana wa Israeli lilifanywa (Kutoka 24;7-8). Mungu aliwaamuru watu wake kujenga mahali patakatifu panapoitwa Hekalu, na kuchagua wanaume toka jamii ya Haruni kuwa makuhani, na kuanza kumtolea sadaka za wanyama kwa ajili ya dhambi zao.

Kitabu cha Mambo ya Walawi kimejaa sheria alizozitoa Mungu katika Mlima Sinai. Zinatoa maelekezo ya Mungu kwa makuhani kuhusu jinsi ya kutoa dhabihu na namna ya kufanya ibada katika Hekalu takatifu. Kitabu pia kinaonyesha jinsi ambavyo Mungu alikubali ibada zilizotolewa kufuatana na maagizo yake na kuzikataa ibada zilizotolewa kinyume na maagizo yake (Mambo ya Walawi 10:1-2).Mambo ya Walawi kimejaa sheria kuhusu jinsi ambavyo wana wa Israeli wanaweza kukubaliwa na kuja katika uwepo wa Mungu, na amri nyingine za makuhani.

Kitabu cha Hesabu ni masimulizi ya ukaidi wa wana wa Israeli wakiwa jangwani. Kina anza na hesabu ya idadi ya watu walioondoka utumwani Misri.Hesabu kinatoa maelekezo ya Mungu kwa ajili ya wana waisraeli watakavyo kaa katika kambi wakati wakiwa wanazunguka jangwani.Kinazungumzia jinsi ambavyo watu watauacha mlima Sinai baada mwaka walipo ondoka Misri na kufika kusini mwa mpaka wa nchi ya Kaanani.Mungu aliwambia kwenda na kuimiliki nchi.Aliwaahidi kuwapa nchi ya Kaanani, lakini waliogopa na hawakumtumaini Mungu kuwa angewapa ushindi. Watu wawili tu, Yoshua na Kalebu, waliamini kwamba Mungu atawapa nchi na waliwasihi watu wote kusonga mbele.Mungu alichukizwa na wana wa israeli kwa kutoakuamini kwao na aliwalaani kwa kuzunguka jangwani kwa miaka arobaini.Katika vizazi vyote vya wana wa Israeli vilivyo toka utumwani, ni Yoshua na Kalebu pekee ndiyo walioingia katika nchi ya ahadi. Wengine wote walifia jangwani kwa kutokuamini kwao (Hesabu 13-14;Zaburi 95:7-11). Hesabu kinatuambia jinsi ambavyo wana waisraeli walikaidi tena na tena wakiwa jangwani mpaka vizazi vyote vya kale vilipokufa.Mwisho, kitabu cha Hesabu kinatoa hesabu ya kizazi kipya cha wa Israeli, wana wa wale waliotoka Misri. Baada ya miaka arobaini ya

kuhangaika jangwani, waisraeli tena wanafika mpakani mwa nchi ya ahadi! Mungu anawapa waisraeli nafasi ya pili!

Kumbukumbu la Torati ni somo ambalo Musa analitoa kwa kizazi kipya cha Waisraeli, kuwaonya wasirudie makosa ya wazazi wao. Anawasihi kumpenda Bwana kwa moyo wao na kuwafundisha watoto wao kufanya hivyo hivyo (Kumbukumbu la Torati 6:4-9).Anawambia kwamba Mungu atawabariki na kuwapa nchi ya kaanani. Anawahakikishia kwamba iwapo tu kama watafanya mapenzi ya Mungu,wataishi kwa muda mrefu katika nchi ya ahadi. Musa anawaonya kizazi hiki kipya wasije waka msahau Bwana kama wazazi wao. Na pia anawaonya wasifanye maagano na ibada za sanamu. Mwisho,Musa anaorodhesha baraka zote ambazo watu watazipata kama watamtii Mungu, na laana zote ambazo zitawajilia kama hawata mtii (Kumbukumbu la Torati 31:24-26).

Wakati Musa anamaliza kuandika Sheria katika Mbao za mawe. Aliwaamuru Walawi kuziweka kando ya sanduku la Agano katika mahali Patakatifu pa Patakatifu pa Hekalu (Kumbukumbu la Torati 31:24-26). Musa akawaamuru makuhani kuisoma sheria kwa watu mara kwa mara, ili kuwakumbusha yale yote Mungu aliyowambia.

Masimulizi ya Kitabu cha Mwanzo,Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati ni misingi kwa uelewa wa Biblia nzima. Kwa kusoma habari hizi tena na tena, watu wa leo watapata uelewa mzuri wa habari zote katika Biblia, Watapata kuelewa Mungu ni Nani, na Jinsi alivyo wa haki na mwenye huruma, ni kwa jinsi gani anapenda kuwa na mahusiano na mwanadamu. Msomaji atapata kuelewa kuhusu asili na tabia ya huyu Muumba, Mungu wa Israeli, Mungu ambaye alimtuma Yesu Kristo aje na kuwa Mwokozi wa mwanadamu.